

# Ukweli thabiti: Uzazi wa Mpango



**Uzazi wa mpango** ni uamuzi wa hiari unaofanywa na mtu binafsi, mke/mume/mwenzi/kijana katika kupanga ni lini wapate watoto, idadi ya watoto, baada ya muda gani na njia ipi ya uzazi wa mpango wangependa kutumia. Kuna aina mbali mbali za njia za uzazi wa mpango na njia hizo ni vidonge, sindano, mipira ya kike na kiume, vipandikizi, kitanzi, upasuaji mdogo, kutofanya ngono na pia njia za asili kama vile kalenda n.k. Uzazi wa mpango pia unajumuisha taarifa kuhusu namna ya kushika mimba inapohitajika na kutibu ugumba. (UNFPA, 2018)

## **Uzazi wa mpango wa hiari**

Utaratibu wa Uzazi wa Mpango kwa hiari unawawezesha wanawake na wanaume kunufaika na haki yao ya uzazi kwa kuamua kwa hiari yao ni lini wapate watoto, idadi ya watoto, baada ya muda gani na njia ipi ya uzazi wa mpango wangependa kutumia. Uzazi wa mpango ni haki ya msingi ya binadamu na haihusiani na dhana potofu kwamba zinalengo la kudhibiti idadi ya watu.

## Mfumo wa kiseru Tanzania

Ipo sera inayosimamia utoaji wa huduma za uzazi wa mpango Tanzania; sera za taifa zimeweka msisitizo katika kusambaza, kuhimarisha mifumo na kutoa vipaumbele kwa matumizi ya njia za uzazi wa mpango.



## Sera za taifa zinazounga mkono utoaji na uenezi wa huduma za uzazi wa mpango

- **Sera ya Idadi ya Watu ya Mwaka 2006:** Inatambua haja ya kuwaelimisha wanawake kuhusu manufaa ya uzazi wa mpango.
- **Sera ya Taifa ya Afya ya Mwaka 2007:** Inasisitiza kuhusu dhamira ya serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi isiyolenga kupata faida na washirika wa maendeleo kuendelea kutoa huduma za afya bure kwa wajawazito, watumiaji wa huduma za uzazi wa mpango na watoto wenye umri chini ya miaka mitano.
- **Mpango Mkakati wa Sekta ya Afya wa Nne wa Mwaka 2015-2020 (Tanzania Bara):** Uzazi wa Mpango umepewa kipaumbele katika kuchelewesha umri wa kuzaa kwa mara ya kwanza, kuhimiza uzazi wa mpango na kuwapa wanawake ridhaa ya kuamua idadi ya watoto wanaotaka kuzaa.
- **Mpango Mkakati wa tatu wa Sekta ya Afya (Zanzibar) wa 2013/14- 2018/19:** Unaelezea haja ya kuboresha upatikanaji wa huduma za uzazi wa mpango kwa kuzingatia watu wengi kutofikiwa na huduma hizo na matumizi kidogo ya njia za kisasa za uzazi wa mpango.
- **Mpango Mkakati wa Pili 2016-2020:** Unaelezea mpango mzima, uboreshaji upatikanaji wa huduma kamili za uzazi wa mpango kwa kuimulika zaidi jamii ya pembezoni na iliyotengwa.

- **Mpango wa Miaka Mitano wa Utekelezaji wa Uzazi wa Mpango 2018-2022 Tanzania Bara:** Ingawa haujazinduliwa, mpango huo unaweka malengo ya kuongeza matumizi ya njia zote za uzazi wa mpango, unazingatia na kujizatiti katika uwekezaji mkubwa unaohimizwa kwa ajili ya mipango mingine ya kimikakati. **Utekelezaji wa uzazi wa mpango (Zanzibar):** Una lengo la kuhimiza matumizi ya uzazi wa mpango na unabainisha maeneo ya kupewa kipaumbele na kiwango cha pesa kinachohitajika.
- **Dira 2025 (Tanzania Bara):** Inaelezea mwelekeo wa Tanzania wa mpito kuanzia nchi inayoendelea hadi kufikia nchi ya pato la kati ifikapo mwaka 2025 ikitilia mkazo katika kuinua kiwango cha maendeleo ya binadamu. Inaelezea umuhimu wa huduma bora za afya ya uzazi na kupunguza kiwango cha sasa cha vifo vya kina mama na watoto wadogo.
- **Dira 2020 (Zanzibar):** Inaelezea mkakati wa kupambana na umaskini na kufikia maendeleo endelevu ifikapo 2020 inayojumuisha uboreshaji wa huduma za afya kwa kina mama na watoto ili kukuza uzazi salama, mpangilio wa uzazi na kupunguza vifo vya watoto.
- **Mpango wa Kitaifa wa Miaka Mitano 2016/17-2020/21 (Tanzania Bara):** Maazimio ya kitaifa ya maendeleo yaliyokubaliwa katika Dira ya mwaka 2025 ikiwa na lengo la kuleta mageuzi kiuchumi nchini kwa kufikia pato la kati na kupiga hatua katika viwanda ifikapo mwaka 2025 huku uzazi wa mpango ukiwa kiungo muhimu cha hatua za kiafya unaozingatia ongezeko la haraka la idadi ya watu linalozidi kukua na linaloweza kuathiri mgawanyiko wa kidemografia. **Mkakati wa Ukuaji na Utokomezaji wa Umaskini Zanzibar 2016-2020 (MKUZA) III):** Unabainisha maazimio ya nchi kuelekea katika pato la kati ifikapo 2020 na upatikanaji wa kutosha wa huduma za uzazi wa mpango ni muhimu kwa mpango wa muda mrefu wa mwelekeo wa kidemografia katika udhibiti ongezeko la idadi ya watu.

## Maazimio ya kikanda na kimataifa

Umoja wa Afrika: "Mpango Endelevu wa Utekelezaji wa Maputo kuhusu Afya na Haki za Uzazi na Kijinsia" (2016-2030), uliorejewa na Kifungu cha 14 (g) katika Itifaki ya Maputo juu ya Haki za Wanawake, ulitoa kipaumbele katika uwekezaji wa kitaifa ili kuhakikisha huduma za uzazi zinawafikia wote ikiwa ni pamoja na matumizi ya njia za kisasa za kuzuia mimba.<sup>1</sup>

Katika mkutano wa kilele wa Uzazi wa mpango uliofanyika London mnamo Julai 11, 2012, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilitia sainsi kwa uzazi wa mpango wa mwaka 2020 na ikaazimia upatikanaji wa huduma bora, mahitaji ya taarifa za uzazi wa mpango kwa hiari.

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilibariki mkutano wa kimataifa wa idadi ya watu na

<sup>1</sup> (Assembly/AU/Dec.601 (XXVI), 2017: Harnessing the Demographic Dividend through Investments in Youth. Available at: <http://wcaro.unfpa.org/sites/default/files/pub-pdf/AU%202017%20DD%20ROADMAP%20Final%20-%20EN.pdf>.



maendeleo mwaka 1994 ambapo serikali ziliafiki kwamba haki za huduma za uzazi wa mpango zitapatikana pale mume na mke na watu binafsi watakapowezechwa kuwa na taarifa na nyenzo sahihi za kuamua idadi, mpangilio na muda wa kupata watoto.

Ajenda ya Maendeleo Endelevu ya Mwaka 2030 (kwa wanachama wa Umoja wa Mataifa ikiwamo Tanzania) inatambua kuwa huduma ya uzazi wa mpango ni haki ya kila mtu binafsi na mume na mke bila kujali mahali au namna wanavyoishi, au wana pato la kiasi gani. Hii ni pamoja na kuondoa vikwazo vyote viwe vya kiuchumi, kijamii au vya kitaasisi dhidi ya kutoa uamuzi kwa werevu na uhuru.

### **Chaguo laweza badili dunia**

Hakuna nchi inayoweza kudai kwamba imefanikiwa kueneza haki ya huduma za uzazi wa mpango kwa watu wote. Bado wanawake wengi wanakabiliwa na kikwazo cha kutokuwa na maamuzi. Na hii ina maana kwamba bado kuna mamilioni ya watu ambao ama wana watoto wengi au wachache kuliko ambavyo wangependa kuwa nao, na hili haliathiri watu binafsi tu bali pia jamii, taasisi, chumi, masoko ya ajira na nchi kwa ujumla.

### **Viwango vya uzazi Tanzania**

Kiwango ambacho mume na mke na watu binafsi wanakuwa na chaguo kuhusu lini kupata watoto, na wangapi na wapishane kwa muda gani kina uhusiano wa moja kwa moja na viwango vya uzazi.


Uzazi ni muhimu kwa watu binafsi kwa sababu inaonyesha namna watu walivyo na mamlaka na nyenzo za kufanya maamuzi yao kuhusu idadi ya watoto, muda na mpangilio wa uzazi. Uzazi ni jambo linalogusa jamii kwa sababu linaweza kukwamisha au kusukuma maendeleo na hatimaye kufikia mafanikio makubwa, sawia na endelevu na ustawi kwa wote.

Wastani wa idadi ya wanawake wenye umri wa kuzaa (kati ya miaka 15 na 49) Tanzania Bara, ikijulikana kama kiwango kamili cha uzazi (TFR), kiko juu kwa 5.2. Tofauti ni ndogo ikilinganishwa na Zanzibar ambako ni 5.1.<sup>2</sup>

<sup>2</sup> Tanzania Demographic and Health Survey (DHS) 2015/16. Available at: <https://dhsprogram.com/pubs/pdf/fr321/fr321.pdf>.

Mahali ambako mume na mke wamewezeshwa kikamilifu, kiwango cha uzazi kinaelekea kujikita katika watoto wawili kwa mwanamke mmoja, kiwango ambacho kinadhaniwa kintoshwa kudhibiti ongezeko la watu mbali na suala la uhamiaji.

Kiwango cha juu cha uzazi kinachangia katika ongezeko kubwa la idadi ya watu na mgawo usio wiana wa watu wenye umri wa miaka 15 au, chini ya hapo. Uzazi endelevu wa kiwango cha juu unamaanisha kwamba ongezeko la vijana wadogo kwa miaka ijayo utasababisha nchi zikabiliwe na uhaba wa pesa zinazohitajika kutoa huduma bora za elimu na afya na zitashindwa kuzalisha fursa za kutosha kwa vijana wanaotafuta ajira chini ya hapo. Uzazi endelevu wa kiwango cha juu unamaanisha kwamba ongezeko la vijana wadogo kwa miaka ijayo utasababisha nchi zikabiliwe na uhaba wa pesa zinazohitajika kutoa huduma bora za elimu na afya na zitashindwa kuzalisha fursa za kutosha kwa vijana wanaotafuta ajira.



### Uzazi kwa vijana Tanzania

Viwango vya mimba za utotoni (miaka 15-10)/ 10-15? vimeshika kasi nchini Tanzania tangu kufanyike Utafiti wa Hali ya Watu na Afya (DHS) kutoka asilimia 23 mwaka 2015/16 hadi asilimia 27 mwaka 2019;<sup>3</sup> hii inamaanisha kwamba kuanzia mwaka 2016 mmoja kwa kila vijana wanne alianza kuzaa. Tofauti mbalimbali za kijiografia zinaonesha kwamba baadhi ya mikoa ina viwango vya juu vya mimba za utotoni vikifikia asilimia 45. Asilimia ya vijana walioanza kuzaa katika visiwa vya Zanzibar ilikuwa ndogo kwa kiwango cha asilimia 8.

Tanzania ni mojawapo ya nchi zenye viwango vya juu vya mimba za utotoni duniani,<sup>4</sup> kwa vijana 132 kwa kila 1,000 wenye umri kati ya miaka 15 na 19.<sup>5</sup> Vijana walioathirika na

<sup>3</sup> Ibid.

<sup>4</sup> The Power of Choice - Reproductive Rights and the Demographic Transition. State of World Population 2018. UNFPA, reports that 132 of every 1,000 live births in Tanzania are to adolescents. Available at: [https://www.unfpa.org/sites/default/files/pub-pdf/UNFPA\\_PUB\\_2018\\_EN\\_SWP.pdf](https://www.unfpa.org/sites/default/files/pub-pdf/UNFPA_PUB_2018_EN_SWP.pdf).

<sup>5</sup> Ibid.



mimba za utotoni pia wanakabiliwa na hali ngumu ya kiuchumi. Madhara yatokanayo na mimba za utotoni kwa pato la taifa Tanzania<sup>6</sup> kwa mwaka ni makubwa, yakifikia upungufu wa asilimia 18. Wakati hasara ya kiuchumi kwa wasichana vijana wanaoacha masomo kwa sababu ya mimba inaweza kufikia dola za Marekani bilioni 5.22 kwa mwaka.<sup>7</sup>

### Kukidhi mahitaji ya kuzuia uzazi

Wanawake wengi wanakuwa na watoto wengi kuliko mahitaji yao kwa sababu uwezo finyu wa kupata huduma waitakayo ya kuzuia mimba, hali inayosababisha mimba zisizotakiwa. Kila mwaka katika nchi zinazoendelea, kunazuka mimba milioni 89 zisizotarajiwa.<sup>8</sup> Nchini Tanzania kiwango cha kuzuia mimba (CPR) kwa njia za kisasa miongoni mwa wanawake walioolewa wakiwa na (miaka 15-49) ni asilimia 32.<sup>9</sup> Hata hivyo, kuna tofauti katika matumizi ya njia za uzazi wa mpango kwenye mkoa mbalimbali kati ya kiwango kidogo cha asilimia 7 Kusini Pemba (Zanzibar) na kiwango cha juu cha asilimia 52 mkoani Lindi. Miongoni mwa wanawake vijana walioolewa wenye umri kati ya miaka 15 na 24, CPR ni ya kiwango kidogo kwa asilimia 16, kwa kati ya asilimia 1 Unguja (Zanzibar) na asilimia 36 mkoani Lindi.<sup>10</sup>

Idadi ya wanawake waliokwishaolewa wenye umri kati ya miaka 15 na 49 ambao hawajapata huduma za uzazi wa mpango, wale wanaotaka kuzaa kwa mpangilio au kusitisha uzazi lakini hawatumii njia za kuzuia mimba – ni asilimia 22, ikitofautiana kati ya mkoa na mkoa. Kiwango cha chini kikiwa kidogo kwa asilimia 10 na kile cha Pemba Kaskazini kikiwa juu kwa asilimia 37.<sup>11</sup>

<sup>6</sup> Motherhood in Childhood: Facing the challenge of adolescent pregnancy. State of World Population 2013. UNFPA. Available at: <https://www.unfpa.org/sites/default/files/pub-pdf/EN-SWOP2013-final.pdf>.

<sup>7</sup> Ibid.

<sup>8</sup> The Power of Choice - Reproductive Rights and the Demographic Transition. State of World Population 2018. UNFPA.

<sup>9</sup> Tanzania DHS 2015/16.

<sup>10</sup> Ibid.


<sup>11</sup> Ibid.



Endapo nchi zinazoendelea zingekidhi mahitaji ya kuzuia mimba kwa njia za kisasa kungekuwa na upungufu wa robo tatu ya mimba zisizokusudiwa (kutoka asilimia 89 ya sasa hadi asilimia 22 kwa mwaka), na kwa mimba zisizotarajiwa (kutoka milioni 30 hadi milioni 7 kwa mwaka), na kupungua kwa utoaji mimba kwa vishawishi (kutoka milioni 48 hadi milioni 12 kwa mwaka).<sup>12</sup>

### Matumizi ya utaratibu wa kisasa kwa mkoa

Asilimia ya wanawake walioolewa wenye umri wa miaka 15 – 49 wanaotumia utaratibu wa kisasa wa uzazi wa mpango



Maelezo yaliyotumika na uwasilishaji wa taarifa kwenye ramani hii kwa vyovyote havimaanishi uelezaji wa maoni kwa upande wa Umoja wa Mataifa, au kuhusu hadhi ya kisheria ya nchi yoyote, jiji au eneo la utawala wake, au kuhusu uwekaji mipaka.

### Huduma ya uzazi wa mpango kwa hiyari itaokoa maisha

Huduma ya uzazi wa mpango kwa hiyari itaokoa maisha, kuboresha afya na kustawisha wanawake na watoto. Ushahidi wa kidunia unaonesha kwamba upunguzaji wa mimba zisizotarajiwa ukichaganywa na huduma kamili kwa wanawake wote wajawazito na watoto wachanga, itapunguza vifo vya kina mama kwa asilimia 73 (kutoka 308,000 hadi 84,000) na upungufu kama huo kwa wastani wa watoto wachanga kutoka milioni 2.7 hadi 538,000 kwa mwaka.<sup>13</sup>

Kiwango cha vifo vya kina mama (MMR) nchini Tanzania, kama kilivyokadiriwa katika utafiti wa karibuni sana wa DHS wa mwaka 2015/16, ni watu 556 kwa kila vizazi

<sup>12</sup> Adding it up: Investing in Contraception and Maternal and Newborn Health. December 2017. Fact Sheet. New York: Guttmacher Institute. Available at: <https://www.guttmacher.org/fact-sheet/adding-it-up-contraception-mnh-2017>.

<sup>13</sup> Starrs, A. M., Ezeh, A. C., Barker, G., Basu, A., Bertrand, J. T., Blum, R., ... Ashford, L. S. Accelerate progress - sexual and reproductive health and rights for all: Report of the Guttmacher-Lancet Commission. The Lancet. DOI: 10.1016/S0140-6736(18)30293-9.



hai 100,000. Hii ina maana kwamba wanawake 11,000 hufa kila mwaka wakati wa ujauzito, kujifungua au katika kipindi cha siku 42 za kuharibika kwa mimba, bila ya kuzingatia chanzo.

Uzazi wa mpango unatoa mwanya kupanga uzazi na unachelewesha wanawake vijana kupata mimba ambazo zinawaweka kwenye hatari ya kudhurika kiafya au kupoteza maisha kutokana na mimba za utotoni na hali kadhalika utazuia wanawake wazee kupata mimba ambazo zingewaweka katika hatari.<sup>14</sup>

### **Jumuisho la uzazi wa mpango wa hiyari na huduma za VVU/Ukimwi**

Mimba zisizotarajiwa na maambukizi ya VVU, vyote vinatokana na kufanya ngono zembe. Mpango shirikishi wa huduma za uzazi wa mpango za hiyari na huduma za VVU/Ukimwi unaweza kuongeza ushawishi wa matumizi ya njia za kuzuia mimba miongoni mwa wateja wa huduma za VVU wanaotaka kuchelewesha mimba, kupanga uzazi au kuweka ukomo wa kushika mimba. Wanawake wanaoishi na VVU hali kadhalika wale walio katika hatari kupata VVU, wanaweza kutumia njia za kuzuia mimba kama vile kondomu ambazo zinazuia mimba na maambukizi ya magonjwa ya zinaa ikiwamo VVU.<sup>15</sup>

### **Manufaa ya kuwekeza katika uzazi wa mpango wa hiyari**

Tafiti zimeonesha kwamba uwekezaji katika Uzazi wa mpango una manufaa makubwa katika maendeleo. Upembuzi umeonesha kwamba upatikanaji wa mahitaji ya kuzuia mimba kwa wanawake wote wanaoishi katika nchi zinazoendelea una manufaa makubwa kuliko gharama iliyotumika; kwani kwa kila dola moja iliyotumika, dola nne huokolewa.<sup>16</sup>

<sup>14</sup> Factsheet. Family Planning/Contraception. 2018. World Health Organization. Available at: <http://www.who.int/news-room/fact-sheets/detail/family-planning-contraception>.

<sup>15</sup> HIV/AIDS: Key Facts: Fact Sheet. World Health Organization. 2018. Available at: <http://www.who.int/news-room/fact-sheets/detail/hiv-aids>.

<sup>16</sup> Starbird E, Norton M and Marcus R. Investing in Family Planning: Key to achieving the Sustainable Development Goals, *Global Health: Science and Practice*, 2016, 4(2): 191-210. Available at: <http://www.ghspjournal.org/content/4/2/191.full.pdf>.



Wakati wanawake na wasichana wanapokuwa na uelewa katika maamuzi yao na kupanga hali yao ya kiafya, uwezo huo utawapa fursa ya kupata elimu bora, kupata ajira nzuri na kufanya maamuzi huru na sahihi katika nyanja mbalimbali za maisha.<sup>17</sup>

Pamoja na kuunga mkono usawa wa kijinsia na kuleta matokeo chanya ya kiafya, familia za kina mama hao na jamii zitaboreka kimapato. Endapo wataamua kuwa na watoto, watakuwa na afya njema na wenye elimu bora, na kuvunja lindi la umaskini linakowakabili mamilioni ya watu na kushusha neema ambayo itaendelea hadi vizazi vijavyo.<sup>18</sup>

Uzazi wa mpango ni mkakati muhimu katika mapambano dhidi ya umaskini na unachangia kuleta maendeleo ya kijamii na kiuchumi katika nchi mbalimbali.

### Uzazi wa mpango wa hiyari unakuza uchumi wa taifa

Upatikanaji wa huduma za uzazi wa mpango baada ya muda unachangia kuwa na watoto wachache wanaowiana na rasilimali za kuwekeza kwa kila mtoto, hali itakayochochea ukuaji wa uchumi kwa kuwezesha mabadiliko kulingana na mpangilio wa umri katika nchi. Kwa kuwa na kiwango kidogo cha uzazi kila mwaka, watu wenye umri wa kufanya kazi katika nchi wanazidi kuongezeka ikilinganishwa na kiwango cha vijana tegemezi. Ongezeko la vijana linatoa fursa ya wakati-mwelekeo ya kukuza uchumi ujulikanayo kama “mgawo wa kidemografia” ambao Umoja wa Afrika umeuchorea ramani (Tume ya Umoja wa Afrika, 2017). Kiwango cha mgawo huo wa kidemografia kwa kiasi unategemea kasi ya kupungua kwa uzazi ambao nao unategemea ni jinsi gani haki za kijinsia na afya ya uzazi kwa wanawake na wasichana zinavyolindwa na jinsi wanawake walivyo na mamlaka. Taarifa na nyenzo za kufanya maamuzi yao kwa uhuru kuhusu lini na mara ngapi washike mimba.

Kwa kuwa na sera za kijamii na kiuchumi zinazowabeba kina mama ikiwa ni pamoja na uwekezaji wenye manufaa kwa wasichana wadogo na kuwawezesha wanawake, nchi zitashuhudia “mgawo wa kidemografia” wenye kukuza uchumi kwa haraka. Makadirio yanaonesha kwamba manufaa ya mgawo wa kidemografia kutokana na uzazi wa mpango yamejitokeza sana katika nchi zenye kiwango cha juu cha uzazi ambako kiwango cha mrejesho wa tija katika uchumi na mapato binafsi unaweza kuzidi asilimia 8 ya pato la taifa ifikapo mwaka 2035.<sup>19</sup>

---

<sup>17</sup> Universal access to sexual and reproductive health—the key to gender equality. UNFPA 2017. Available at: <https://www.unfpa.org/press/universal-access-sexual-and-reproductive-health%E2%80%94key-gender-equality>.

<sup>18</sup> Starbird E, Norton M and Marcus R. Investing in Family Planning: Key to achieving the Sustainable Development Goals, *Global Health: Science and Practice*, 2016, 4(2): 191-210. Available at: <http://www.ghspjournal.org/content/4/2/191.full.pdf>.

<sup>19</sup> Stenberg K, Axelson H, Sheehan P, Anderson I, Gülmezoglu AM, Temmerman M, et al. Study Group for the Global Investment Framework for Women’s Children’s Health. Advancing social and economic development by investing in women’s and children’s health: A New Global Investment Framework. *Lancet*. 2014;383 (9925):1333-1354. CrossRef. Medline.

## Uzazi wa mpango wa hiyari kama sehemu ya kutambua ajenda 2030

Ajenda ya Maendeleo Endelevu ya 2030 inatambua afya ya uzazi na haki kama lengo maalum chini ya mojawapo ya malengo 17 ya Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) na ndilo lengo kuu kati ya yote. Kiwango cha juu cha uzazi na ongezeko la haraka la watu, vinaweza kuathiri mafanikio katika utekelezaji wa malengo hayo. Kwa mfano, baadhi ya nchi zinaweza kushindwa kutekeleza lengo namba 1 kuhusu kutokomeza umaskini, lengo namba 3 kuhusu huduma bora za afya na ustawi wa jamii na malengo mengine yahasuyo miji endelevu na upatikanaji wa kazi bora kwa wote.<sup>20</sup>



## Huduma za uzazi wa mpango kwa wengi waliotelekezwa

Kuna dhana inayoenea kwamba ukuaji wa uchumi pekee hautoshi kutokomeza umaskini kama si shirikishi.<sup>21,22</sup> Ajenda ya Maendeleo Endelevu ya mwaka 2030 inabainisha kwamba afya ya jinsia na uzazi na haki kama lengo maalum kwa kila mtu binafsi na mume na mke bila ya kujali wapi au jinsi wanavyoishi, au wana kipato gani. Hii ni pamoja na kutokomeza vikwazo vyote – vya kiuchumi, kijamii au kitaasisi – vinavyozuia watu kufanya maamuzi huru na ya uelewa.<sup>23</sup>

Maendeleo makubwa yamepatikana katika kutetea haki ya uzazi. Hata hivyo hakuna nchi inayoweza kudai kwamba makundi yote ya watu yananufaika na haki hii wakati wote. Kila nchi inahitaji kubainisha mseto wa huduma na rasilimali zinazohitajika ili kulinda haki ya uzazi kwa raia wote, ikihakikisha kwamba hakuna anayeachwa nyuma, na kutokomeza vikwazo vinavyowazuia mume na mke na watu binafsi kufanya maamuzi kwa uhuru na kiwajibikaji kuhusu idadi ya watoto wa kuzaa na muda wa kuzaa. Kama jitihada hazitafanyiwa kazi katika eneo hili hayataweza kufikiwa.

<sup>20</sup> The Power of Choice - Reproductive Rights and the Demographic Transition. State of World Population 2018. UNFPA.

<sup>21</sup> Bourguignon, François. 2004. "The Poverty-Growth-Inequality Triangle." Poverty, Inequality and Growth 69: 342674-120611890151.

<sup>22</sup> Bourguignon, François. "The Growth Elasticity of Poverty Reduction: Explaining Heterogeneity across Countries and Time Periods." Inequality and Growth: Theory and Policy Implications 1, no. 1 (2003).

<sup>23</sup> The Power of Choice - Reproductive Rights and the Demographic Transition. State of World Population 2018. UNFPA.

# Ushuhuda wa mafanikio

## **Mipango ya kuwafikia watu wote ya afya ya uzazi: Hakuna anayeachwa nyuma**

Joyce Albert ni muuguzi aliyesajiliwa katika Zahanati ya Kirumba, Mwanza. Yeye pamoja na mwenzake wanaosha na kusugua mikono yao kwenye sinki na kuvaa glavu zao ili kumhudumia Minza. Joyce anasafisha mkono wa Minza, mwenzake anampa Minza dawa ya ganzi na kisha anaingiza kinga ya mimba chini ya ngozi kwenye mkono wa Minza. Joyce anamfuta mkono Minza na dakika chache baadaye Minza anarudi nyumbani akiwa hana wasiwasi na kitu kimoja - mimba ambayo hayupo tayari kuwa nayo.

Kipandikizi ni kijiti kidogo ambacho kinaingizwa chini ya ngozi na hutoa kinga dhidi ya mimba kwa miaka mitatu. Kikiondolewa, uzazi unarudi katika hali ya kawaida.

Minza anaishi katika makazi yasiyo rasmi karibu na Zahanati ya Kirumba na ni mmoja wa wateja zaidi ya 1,000 waliohudhuria programu hiyo ya kuifikia jamii mwishoni mwa Juni 2016. Bila programu hiyo Miza angepaswa kusafiri kwenda kwenye kituo cha afya, umbali wa kilomita mbili. Umbali hadi kwenye kituo cha afya huwakatisha tamaa wanawake wengi kutafuta huduma za hiyari za uzazi wa mpango. Programu ya kuifikia jamii huleta haki hizi kwa watu na mwitikio wake ulikuwa mkubwa.

Mpango wa kuwafikia watu, kama sehemu ya njia pana ya Huduma ya Uzazi, Mama, Watoto Wachanga na Afya ya Mtoto (RMNCH) ni mfano mzuri wa mchanganyiko wa huduma na rasilimali inayohitajika ili kuchangia haki za uzazi za wananchi wa Tanzania. Minza anaendesha genge na hawezi kuliacha na kutumia saa tatu katika kituo cha afya. Joyce anaelezea: "Hapa anaweza kumpata mtu wa kumshikia foleni huku anahudumia genge lake sokoni. Anakuja tu wakati wamebaki watu wawili au watatu mbele yake kwenye foleni."

Huduma unganifu za RMNCH kupitia mpango wa kuifikia jamii, ambazo zinajumuisha uzazi wa mpango wa hiyari, ni jambo muhimu la kusaidia kuisaidia Tanzania kufikia malengo yake ya afya ya uzazi. Mpango wa kuwafikia watu ni muhimu; hutoa elimu na njia za uzazi wa mpango kwa wanawake na wenzi wao ili kuwajibika katika kuamua idadi, nafasi na muda wa watoto wao.

"Mpango wa kuifikia jamii ni moja ya njia za nguvu na bora zaidi ya kuwafikia watu wanaohitaji huduma za uzazi wa mpango. Si wanawake wote wanaweza kufika kliniki, hivyo lazima kukutana nao pale walipo. Sisi hupeleka huduma kwenye baadhi ya jamii zilizo mbali na zisizohudumiwa ipasavyo nchini, na hivyo kuwapa chaguo watu ambao hawawezi kuja kwetu," anasema Francis Omorge, Meneja wa Tawi, DKT Mwanza.



### Istilahi za Uzazi wa Mpango

**Ukubwa wa kiasi cha njia za kuzuia uzazi** ni asilimia ya wanawake ambao hivi sasa wanatumia, au ambao mwenzi wake anatumia hivi sasa, angalau njia mojawapo ya kuzuia uzazi, bila kujali njia anayotumia. Mara nyingi huripotwa kwa wanawake walioolewa au wanaoshi kinyumba wenye umri wa miaka 15 hadi 49.

**Uwezo mkubwa wa kuzaa** kwa ujumla inahusisha kiasi cha uwezo wa kuzaa zaidi ya mara nne kwa kila mwanamke. Kunapokuwa hakuna vifo vingi au kiasi kikubwa cha uhamaji, kiasi cha juu cha uzalishaji kinamaanisha ukuajia wa haraka wa idadi ya watu.<sup>24</sup>

**Uwezo mdogo wa kuzaa** inahusisha kiasi cha jumla cha uwezo wa kuzaa chini ya mara 1.5 kwa kila mwanamke. Kiasi hiki ni chini ya kiwango kinachotakiwa kuhimili ukubwa wa sasa wa idadi ya watu.<sup>24</sup>

**Uwezo wa kati wa kuzaa** inahusisha kiasi cha kuzaa kati ya mara 2.5 na 3.9.<sup>24</sup>

**Njia za kisasa za kuzuia uzazi** inahusisha kuhasiwa kwa mwanamke na mwanaume, vidonge vya kumeza vya homoni, Kitanzi (IUD), kondomu ya kiume, sindano, vipandikizi, kondomu ya kike na kuzuia uzazi kwa dharura.

**Uwezo mbadala wa kuzaa** inahusisha kiasi cha jumla cha kuzaa mara 2.1 kwa kila mwanamke ambao utafanya ukuaji wa idadi ya watu ubaki vile vile.<sup>24</sup>

**Kiasi cha Jumla ya uwezo wa kuzaa** ni idadi ya wastani ya watoto wanaozaliwa wakiwa hai kwa mwanamke anayeweza kuendelea kuishi katika muda wake wa kuzaa (huishi miaka 15 to 49).

**Hitaji lililokidhi la uzuiaji uzazi** ni idadi au asilimia ya wanawake ambao hivi sasa wameolewa au wanaishi kinyumba ambao wapo kwenye miaka yao ya kuzaa watoto, lakini ambao kwa sasa hawatumii njia ya kuzuia uzazi.

<sup>24</sup> Ibid.